



## **Maswali Ambayo Huulizwa Mara Nyingi Kuhusu Usajili wa Shule ya Awali**

**SWALI: Mtoto wangu atakuwa na umri wa miaka 4 baada ya muda wa usajili. Je ninaweza bado kusajili mtoto wangu katika muda huo ili aongezwe katika bahati nasibu?**

*JAWABU: Ndiyo, Iwapo mtoto wako atatimiza umri wa miaka 4 kufikia au kabla ya Septemba 1, 2021, mtoto wako anastahiki kuingia shule ya awali kwa mwaka wa shule wa 2021-2022.*

**SWALI: Nikimsajili mtoto wangu katika siku ya kwanza ya usajili, nitapata chaguo langu la kwanza au shule ninayopendelea?**

*JAWABU: Siyo lazima. Wanafunzi wote wanaokamilisha fomu ya usajili na wanaowasilisha hati kati ya Machi 8, 2021 na Machi 28, 2021 watapokea nambari ya bahati nasibu isiyojulikana au isiyopangiwa. Kumsajili mtoto wako katika siku ya kwanza au mwisho ya usajili haina athari kwa uteuzi wa nambari hiyo isiyejulikana ya bahati nasibu. Nambari ya bahati nasibu unayopewa ikiwa dogo zaidi, una uwezekano zaidi wa kukubaliwa kulingana na chaguo lako la kwanza, lakini wakati unapojisajili katika muda wa kujisajili hauna athari katika nambari hii ya bahati nasibu.*

**SWALI: Je nini itatendeka nisipowasilisha hati zote zinazotakiwa kabla muda wa usajili ufungwe?**

*JAWABU: Usajili pekee unaoambatana na hati zote zinazohitajika kwa usajili utapoke nambari ya bahati nasibu. Usajili usiyo kamilishwa utawekwa katika orodha ya wanaoongoja kulingana na tarehe usajili na hati zinazoambatana zimekamilishwa.*

**SWALI: Je ninaweza kujisajili kabla ya muda wa usajili wa shule ya awali (Machi 8-28)?**

*JAWABU: Ndiyo, lakini tafadhali kumbuka kwamba mtu yeyote anayewasilisha usajili na hati zinazoahitajika baada ya Machi 28 watawekwa katika orodha ya wanaoongoja na watapangiliwa baada ya kutolewa kwa barua rasmi za uteuzi kwa shule zimetolewa kulingana na upatikanaji wa nafasi na tarehe ya usajili. Idara ya Utoto wa Awali huwa na orodha ya wanaoongoja ya mwisho kabisa.*

**SWALI: Je ninahitaji kusajili mtoto wangu wa shule ya awali iwapo amejisajili sasa katika Lowell Public Schools akiwa na IEP (Mpango wa Elimu wa Kibinafsi) ya kurejelea shule ya awali katika mwaka wa shule wa 2021-22?**

*JAWABU: Hapana. Wanafunzi wa shule ya awali wanaorejelea kwa mwaka wa pili wa shule ya awali hawahitaji kusajili upya mtoto wao. Lakini, tafadhali kumbuka kwamba wanafunzi wote waliosajiliwa katika programu ya sasa ya shule ya awali ya Lowell Public Schools wanaojisajili kwa chekechea wanafaa kujisajili upya kwa mwaka wa shule wa 2021-2022.*

**SWALI: Je nini itafanyika iwapo sitapata shule niliyotaka?**

*JAWABU: Watu wote wanaojisajili watapatiwa nambari ya bahati nasibu wanapopokea barua ya kukubaliwa kupitia barua pepe iliyo na maelekezo ya kina kuhusu hatua zifuatazo. Ni lazima wazazi/walezi wote wajibu arifa hiyo huku wakichagua mojawapo ya chaguo zifuatazo:*

*1. Kukubali mpangilio*

2. Kukubali mpangilio lakini kuwekwa katika orodha ya wanaoongoja ili kuongoja shule unayopendelea.
3. Kukataa mpangilio na kubaki katika orodha ya wanaoongoja ili kuongoja shule unayopendelea; au
4. Kukataa mpangilio na kutafuta mpango mwingine wa shule ya awali.

**SWALI: Je ni nini itatendeka nikichagua kipindi cha siku kamili katika chaguo langu la vipindi, lakini shule yangu ninayopendelea ina vipindi vya asubuhi au jioni?**

*JAWABU: Kukubaliwa kwa shule unafanywa kulingana na nambari za bahati nasibu na shule zinazopendelewa na hazina uhusiano na vipindi vinavyopendelewa.*

**SWALI: Je kuwa kwa ndugu yake mkubwa katika shule hiyo itahakikisha mtoto wangu wa shule ya awali atapata nafasi katika shule hiyo hiyo?**

*JAWABU: Hapana. Kwa bahati mbaya, kupendelea uwepo wa ndugu haitumiki katika shule ya awali. Uteuzi wa shule ya awali kwa shule unafanywa kulingana na nambari za bahati nasibu. Usajili kwa shule ya awali ni kwa mwaka mmoja pekee.*

**SWALI: Je mwanafunzi wangu wa shule ya awali ataweza kupata basi kwenda na kurudi kutoka programu ya shule ya awali?**

*JAWABU: Hapana. Usafirishaji haupatikani kwa wanafunzi wa shule ya awali. Wanafunzi wa shule ya awali walio na Mpango wa Elimu ya Kibinafsi (IEP) pekee iliyo na usafirishaji watapata usafirishaji.*

**SWALI: Je shule zote hutoa shule ya awali?**

*JAWABU: Hapana. Chaguo za siku kamili zinapatikana katika Cardinal O'Connell Early Learning Center na the Greenhalge Elementary School. Iwapo ungependa kuongezwa katika bahati nasibu ya programu ya siku kamili, ni lazima uchague mojawapo ya shule hizi 2.*

**SWALI: Je nini itafanyika iwapo sitapokea arifa ya uwezekano wa kukubaliwa katika shule ya awali?**

*JAWABU: Ilani zote zitatumwa kwa anwani ya barua pepe iliyotumika kumsajili mtoto wako. Tafadhali angalia sehemu zozote za spam/junk. Hifadhi nakala ya barua pepe ya kuhakikisha usajili kwa vile itakuwa na rekodi ya nambari ya PR (usajili wa kibinafsi) na tarehe ya kuwasilisha hati. Iwapo hujapokea uhakikishaji au taarifa yeyote, tafadhali wasiliana na Idara ya Utoto wa Awali kupitia 978-674-2050.*

**SWALI: Je nini itafanyika iwapo sitajibu arifa ya kukubaliwa katika shule ya awali? Je mtoto wangu bado ataweza kuhudhuria shule ya awali ya LPS katika Septemba?**

*JAWABU: Inawezekana. Iwapo hutatoa jibu katika arifa ya kukubaliwa katika muda unaofaa, nafasi hiyo inaweza kupatiwa kwa watoto wengineo walio katika orodha ya wanaoongoja. Familia wowote wasio jibu arifa wanaweza kuongezwa katika orodha ya wanaoongoja.*

**SWALI: Je mtoto wangu ataingia chekechea bila usajili katika shule yao ya awali?**

*JAWABU: Hapana. Ni lazima wanafunzi wote wajisajili kwa chekechea. Shule ya awali ni ya mwaka 1 pekee, na haina uhusiano na usajili wa chekechea. Tarehe za usajili wa chekechea zitatangazwa katika tarehe zingine baadaye. Taarifa zaidi kuhusu usajili wa chekechea utachapishwa katika tovuti ya Lowell Public Schools.*